


# Minyoo ya Mbwa

Mbwa huwa na minyoo ambayo hudhuru afya yao. Minyoo hawa pia hudhuru binadamu na mifugo. Iwapo mbwa ana mimba, anaweza ambukiza watoto wake minyoo hawa. Minyoo hawa hufanya mbwa wakonde na wadhaifu kwa kunyonya viini vya chakula.



Minyoo hawa huingia kwa mazingira kupitia kinyesi cha mbwa.

Watoto wachanga wako kwa hatari kubwa ya kupata hawa minyoo kwa sababu hao ndio hukaa na mbwa sana.

## Chunga mbwa wako ili uhifadhi afya yako.

Zika ama choma kinyesi cha mbwa.

Nawa mikono kila wakati baada ya kuzika ama kuchoma kinyesi cha mbwa.



Vaa viatu kila wakati.

Patia mbwa mkubwa dawa ya minyoo baada ya miezi mitatu. Kwa mbwa wadogo, wape dawa ya minyoo kila mwezi.



Usilishe mbwa wako nyama ambaye haijapikwa au iliyo laaniwa. Linda mbwa wako asije akazurura na kukula nyama mbichi.

Kwa maswali kuhusu afya ya mbwa wako, piga simu kwa daktari wa mifugo wa kaunti: \_\_\_\_\_

## Aina ya minyoo wa mbwa ambao wanaweza kukuambukizwa na jinsi ya kujikinga

Kikundi cha minyoo	Majina ya kisayansi ya minyoo	Jinsi inavyoambukizwa	Jinsi ya kuzuia mbwa au binadamu kuambukizwa
Hookworms	<i>Ancylostoma caninum</i>	Mbwa anayenyonyesha na hajapata dawa ya minyoo anaweza kupitisha minyoo kwa wanao kupitia kwa maziwa.  Mayai ya minyoo hupitishwa kwa kinyesi na kuingia kwa mazingira yetu.	Patia mbwa mjazito dawa ya minyoo kabla hajazaa ili kuzuia minyoo kupata wanawe kupitia tumbo la uzazi ama kwa maziwa wanaponyonyeshwa. Patia mbwa wako dawa ya minyoo kila baada ya miezi mitatu.
		Minyoo huingia kwa miili ya binadamu kupitia ngozi.	Vaa viatu vilivyofungwa ukiwa nje ya nyumba.
	<i>Unicinaria sp.</i>		
Roundworms	<i>Toxocara canis</i>	Mbwa anayenyonyesha na hajapata dawa ya minyoo anaweza kupitisha minyoo kwa wanao kupitia kwa maziwa.  Mayai ya minyoo hupitishwa kwa kinyesi na kuingia kwa mazingira yetu.	Patia mbwa mjazito dawa ya minyoo kabla hajazaa ili kuzuia minyoo kupata wanawe kupitia tumbo la uzazi ama kwa maziwa wanaponyonyeshwa.  Patia mbwa wako dawa ya minyoo kila baada ya miezi mitatu.
		Binadamu wanaweza pata minyoo hawa wasiponawa mikono baada ya kushika kinyesi cha mbwa au kushika mchanga.	Nawa mikono yako baada ya kushika mchanga ama kinyesi cha mbwa.  Usile nyama mbichi.
	<i>Strongyloides</i>	Minyoo hawa wanaweza patikana kwa nyama mbichi ama nyama ambayo haijapikwa kikamilifu.	Pika nyama na uhakikishe imeiva vizuri kabla ya kukula.
Tapeworms	<i>Dipylidium caninum</i>  <i>Echinococcus sp.</i>	Mbwa wanaweza pata minyoo hawa kwa kukula viroboto ama kwa kukula nyama mbichi.  Minyoo hawa wanaingia kwa mazingira yetu kupitia kwa kinyesi cha mbwa ambaye hajapewa dawa ya minyoo.	Usilishe mbwa nyama mbichi. Patia mbwa wako nyama iliyopikwa vikamilifu.  Lisha mbwa wako vizuri ndiposa asikule nyama mbichi anayowinda.  Patia mbwa wako dawa ya minyoo baada ya kila miezi mitatu.
		Binadamu hupata hawa minyoo kutoka mazingira machafu wanapokosa kuosha mikono ama kutoka kwa viroboto.	Nawa mikono yako baada ya kushika kinyesi cha mbwa ama kutoka shambani. Pika nyama yako vizuri na usile nyama mbichi ama ambayo haijaiva vikamilifu.
	<i>Taenia sp.</i>  <i>Spirometra sp.</i>		
Protozoa	<i>Giardia</i>  <i>Cryptosporidium</i>	Mayai ya minyoo yanapitisha kwa kinyesi cha mbwa ambaye hajapewa dawa ya minyoo kisha yanaingia kwa mazingira ama maji. Haya mayai yanaweza patikana kwa nyama ambayo haijapikwa vizuri ama maji machafu wakati mbwa anakula vyakula hivyo au kunywa hayo maji machafu.	Usilishe mbwa nyama mbichi. Patia mbwa wako nyama iliyopikwa.  Patia mbwa wako maji safi na vyakula safi.  Patia mbwa wako dawa ya minyoo baada ya miezi mitatu.
		Binadamu hupata mayai ya minyoo kupitia maji machafu, chakula chafu ama kwa mikono chafu.	Osha mboga na matunda vizuri.  Kula vyakula ambavyo vimepikwa na vikaiva.  Nawa mikono yako kila wakati haswa baada ya kushika kinyesi cha mbwa.
	<i>Neospora</i>		

**Fuata maagizo haya ili kuzuia mbwa wako na familia yako kupata magonjwa yanayoletwa na minyoo ya mbwa**

**ILRI** INTERNATIONAL LIVESTOCK RESEARCH INSTITUTE



UNIVERSITY OF  
**LIVERPOOL**